**HOTUBA YA MHE. RIDHIWANI KIKWETE (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA WAKATI WA KUFUNGA KIKAO KAZI CHA SITA (6) CHA SERIKALI MTANDAO TAREHE 19 FEBRUARI, 2026 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.**

**Mhe. Amos Makalla,** Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

**Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro,** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala, Katiba na Sheria

**Ndg. Mululi Mahendeka;** Katibu Mkuu Ikulu

***Makatibu Wakuu wote,***

***Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya,***

***Dkt. Mussa Kisaka;*** *Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Wakurugenzi*** *wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,*

***Wakuu wa Idara*** *za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali*

***Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo/Sehemu,*** *na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;*

**Viongozi wa Dini,**

**Waandishi wa Habari**,

*Itifaki imezingatiwa;*

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

Awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutuwezesha kukutana hapa na kufanikisha **Kikao Kazi hiki cha sita cha Serikali Mtandao**, ambacho tunakihitimisha rasmi hii leo.

Napenda pia kutoa **shukrani za dhati** kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa maandalizi mazuri na uratibu madhubuti uliowezesha kikao hiki kufanyika kwa mafanikio makubwa. Shukrani za kipekee ziende kwa wadhamini wote ambao mmewezesha kufanikiwa kwa kikao hiki. Vilevile, nawapongeza washiriki wote kwa kujitokeza kwa wingi, kushiriki kikamilifu na kuchangia mijadala yenye tija kwa maendeleo ya Serikali Mtandao nchini.

**Ndg. Washiriki;**

Kikao Kazi hiki cha siku tatu, kimewakutanisha takribani washiriki 1,000 kutoka sekta za umma na binafsi, na kimejadili kwa kina masuala muhimu yanayohusu **ujenzi, uendelezaji na usimamizi wa jitihada za Serikali Mtandao**. Kupitia mijadala hii, tumepata fursa ya:

- Kutathmini utekelezaji wa maazimio ya Kikao Kazi kilichopita,
- Kubainisha mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya TEHAMA Serikalini,
- Kujadili changamoto zilizopo na kuweka mikakati ya pamoja ya kukabiliana nazo,
- Na kuweka maazimio mapya yatakayotuongoza katika hatua zinazofuata za kuendelea kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma za umma kwa njia ya kidijitali.

Nimefarijika kuona kuwa, mijadala yote imejikita katika **uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao**, jambo ambalo ni msingi muhimu wa kuhakikisha miradi ya TEHAMA Serikalini inakuwa salama, endelevu na yenye kujali mahitaji na matakwa ya wananchi.

**Ndg. Washiriki;**

Katika kikao kazi hiki, Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), itatoa tuzo kwa taasisi zilizofanya vizuri katika kuzingatia **Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao,** kwenye utekelezaji wa miradi ya TEHAMA. Napenda kutumia fursa hii kuzipongeza taasisi zote zitakazotunukiwa tuzo hizi. Tuzo hizi si za heshima tu, bali ni chachu ya kuhamasisha ubora, uwajibikaji na uzingatiaji wa misingi ya Serikali Mtandao katika taasisi zote za umma.

Kimsingi tuzo hizi zinalenga:

- Kukuza utamaduni wa uzingatiaji wa sheria na viwango,
- Kuhamasisha ubunifu na matumizi bora ya rasilimali za umma,
- Kupunguza urudufu wa miradi ya TEHAMA Serikalini,
- Na kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inachangia kikamilifu katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

**Ndg. Washiriki;**

Kikao hiki pia kimetumika kama jukwaa muhimu la kujadili **Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka 50 katika eneo la Serikali Mtandao** hasa katika eneo la ubunifu na matumizi ya teknolojia. Mawazo mliyoyatoa nina imani yataiwezesha Serikali kutekeleza dira hii katika kuijenga Serikali ya kidijitali iliyo jumuishi, salama, inayotumia teknolojia za kisasa, ikiwemo Akili Mnemba, IOT na Blockchain katika utoaji wa huduma.

Napenda kusisitiza kuwa, utekelezaji wa dira hii unahitaji ushirikiano wa karibu kati ya Serikali, sekta binafsi, wadau wa maendeleo na wananchi kwa ujumla.

**Ndg. Washiriki;**

Kwa niaba ya Serikali, nawahakikishia kuwa maazimio yote yaliyofikiwa katika kikao kazi hiki yatafanyiwa kazi kwa karibu, kwa kushirikiana na taasisi husika chini ya usimamizi wa Wizara yangu na uratibu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, ili kuhakikisha kuwa maazimio haya yanatekelezwa kwa wakati. Aidha, Serikali itaendelea kutumia

majukwaa kama haya kufuatilia utekelezaji, kusikiliza changamoto na kuimarisha ushirikiano baina ya wadau wote wa Serikali Mtandao.

Kwa heshima ya kipekee, napenda kumshukuru **Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan**, kwa maono yake, uongozi thabiti na uwekezaji mkubwa katika sekta ya TEHAMA, ambao umeendelea kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa katika safari ya kuijenga Serikali Mtandao ya kisasa, salama na jumuishi.

Mwisho, napenda kuwashukuru tena Washiriki wote, Wadhamini na Uongozi wa Mkoa wa Arusha kwa ushirikiano mkubwa na mapokezi mazuri yaliyowezesha kikao kazi hiki kufanikiwa.

Nawatakia safari njema mnaporejea katika maeneo yenu ya kazi, muendelee kuwa mabalozi wazuri wa mageuzi ya kidijitali Serikalini.

**Kwa maneno hayo machache, natangaza rasmi Kikao Kazi hiki cha Sita cha Serikali Mtandao kimefungwa.**

*Asanteni sana kwa kunisikiliza.*

***Kazi na Utu………………….***